

**SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA**

(SURA YA 290)

**SHERIA NDOGO**

Zimetungwa chini ya Kifungu Cha 6 (1) na 16(1)

**SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI KOROGWE  
ZA MWAKA 2010**

- |                            |   |  |
|----------------------------|---|--|
| Jina na mwanzo wa kutumika | 1 | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Korogwe za mwaka 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la serikali.   |
| Eneo la matumizi           | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe.  |
| Tafsiri                    | 3 | <p>Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-</p> <p>“Ada” Maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali na Leseni mbalimbali zitolewazo;</p> <p>“Afisa muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;</p> <p>“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Korogwe.</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Mji wa Korogwe pamoja na afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;</p> <p>“Kibali cha ujenzi “ maana yake ni kibali cha ujenzi kinachotolewa na Halmashauri;</p> <p>“Maeneo ya Kati” maana yake ni maeneo yaliyopo katikati ya Mji yaani Central Business District (CBD);</p> |
| Ada na ushuru              | 4 | <p>(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwaajili ya huduma, vibali na Leseni zitolewazo kama ilivyoorodheshwa kwenyejedwali la Sheria Ndogo hizi.</p> <p>(2) Ada na ushuru utozwao chini ya Sheria hizi Ndogo utalipwa kabla ya mwombaji kupata huduma au leseni au kibali husika na italipwa</p>   |

kabla au tarehe 30 ya mwezi Juni ya mwaka unaolipwa.

Wajibu wa  
kulipa ada na  
ushuru

5 Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada na au ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kulipa ada na au ushuru kama zilivyoelekezwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

5 (1) Ada na Ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi yenye nembo ya Halmashauri.

(2) Mtu yeyote aliyelipa ada na au ushuru atatakiwa kudai stakabadhi na atatakiwa kuionyesha kwa Afisa Muidhiniwa mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(3) Hautakuwa ni utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi.

6 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyo zidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha  
kosa

7 Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyo zidi shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa faini iliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

